

## **MKATABA WA KUPANGISHA SEHEMU YA BIASHARA**

MKATABA HUU umefanyika leo tarehe 26 / 07 / 2024

### **BAINA YA**

**JUMA ALLY MUSSA** Wa S.L.P 121 Mtaa wa CHAMAKWEZA, Kata ya CHALINZE, Wilaya BAGAMOYO Mkoa wa PWANI, (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MWENYE JENGO**”) kwa upande mmoja,

### **NA**

**TANZANIA ANSHUN MINING NEW DEVELOPMENT COMPANY LIMITED**

PWANI, (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**Mpangaji**” kwa upande mwingine.

### **KWA KUWA: -**

- a) Mwenye jengo ni mmiliki halali wa Jengo la biashara lililojengwa katika Mkoa wa pwani, wilaya ya bagamoyo.
- b) Mwenye jengo anayo nia ya kupangisha **CHUMBA CHA OFISI** jengo hilo,mpangaji anayo nia ya kupanga sehemu tajwa hapo juu kwa makubaliano yafuatayo.

### **MKATABA HUU unashuhudia yafuatayo: -**

1. Kwamba mwenye jengo atampangisha mpangaji sehemu tajwa hapo juu kwa kodi ya shilingi 1,000,000(milliom moja) Kwa kila mwaka kwa miaka mitatu kuanzia tarehe 26/07/2024 hadi tarehe 26/07/2027.
2. Kwamba mpangaji wakati wa kusaini mkataba huu atamlipa mwenye jengo kodi ya miaka mitatu (03) ambayo ni sawa na shilingi 3,000,000 (million tatu).

### **MPANGAJI ANAAHIDI na kuthibitisha kama ifuatavyo: -**

3. Kwamba atatumia sehemu hiyo Kwa shughuli za kibiashara tu.
4. Kwamba hatafanya mabadiliko ya kudumu kwenye sehemu hiyo bila kibali cha maandishi toka Kwa mwenye jengo.